



JAMHURI YA KENYA

WIZARA YA MAFUTA NA UCHIMBAJI MADINI

MKATABA WA HUDUMA KWA WANANCHI

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
---------	--------------------	--------------------------	------------	----------------------

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
1.	Kuandaa na kufikisha kwa NEMA idhini za matakwa ya ujenzi wa vituo vya mafuta	Kupata ripoti kuhusu athari za kimazingira na kijamii kutoka NEMA	Hakuna malipo	Siku ishirini na moja (21)

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
2.	Kutoa habari/taarifa kwa wawekezaji	Barua/hati ya maombi inayoonyesha habari/taarifa inayohitajika	Hakuna malipo	Siku kumi na nne (14)
3.	Kuidhinisha utoaji wa nafasi kwa wawekezaji wapya katika ugawaji wa kiasi kinachopotea kutokana na uvukizi au uvujaji, kulingana na utaratibu wa KPC	<ul style="list-style-type: none"> • Leseni kutoka kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Petroli (EPRA) ya uagizaji /uuzaji nje ya nchi na uuzaji wa kijumla wa bidhaa za petroli • Mkataba wa makubaliano kuhusu usafirishaji na uhifadhi uliokubaliwa na Kampuni ya Bomba ya Kenya (KPC) • Taratibu ya zabuni wazi iliyotiwa sahihi kwa kuzingatia sheria na masharti yaliyowekwa 	Hakuna malipo	Siku saba (7)

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
4.	Uandaaji /utayarishaji wa maombi ya leseni za taraja	<ul style="list-style-type: none"> Barua inayoonyesha eneo lililotambuliwa Ombi rasmi la leseni ya eneo lililotambuliwa Wasilisha anwani ya kampuni, nakala ya cheti cha usajili, maelezo ya kiufundi na kifedha 	Hakuna malipo	Siku tisini (90)
5.	Leseni ya taraja (utoaji mpya) kipindi cha awali cha miaka mitatu	<ul style="list-style-type: none"> Tuma ombi mtandaoni kupitia tovuti ya uchimbaji madini (Mining Cadaster portal) 	Shilingi elfu hamsini (50,000), shilingi elfu mbili mia tano (2,500) kwa kila kilomita moja mraba, elfu hamsini (50,000) kwa mwaka	<p>Kuidhinishwa kwa kukataa katika muda wa siku tisini.</p> <p>Arifa kati ya siku ishirini na moja ili mwombaji kukubali ama kukataa/kughairi leseni</p> <p>Leseni kutolewa katika siku ishirini na moja (21) baada ya kuchapishwa.</p>

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
6.	Leseni ya uchimbaji madini (kipindi kisichozidi miaka ishirini na mitano)	Tuma ombi mtandaoni kupitia tovuti ya uchimbaji madini (Mining Cadaster portal)	<p>Ada ya maombi ya shilingi elfu hamsini (50,000)</p> <p>Kodi ya ardhi ya Shilingi elfu mbili (2,000) kwa hekta kiwango cha chini kikiwa shilling elfu mia tano (500,000)</p>	<p>Kuidhinishwa ama kukataliwa kwa muda usizidi siku mia moja ishirini (120) baada ya kutuma maombi</p> <p>Arifa ya muda wa siku thelathini (30) baada ya kuidhinishwa.</p> <p>Leseni kutolewa siku arobaini na tano (45) baada ya kuchapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali na magazeti ya kila siku.</p>

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
7.	Kibali cha taraja cha awamu ya miaka mitano (5)	Tuma ombi mtandaoni kupitia tovuti ya uchimbaji madini (Mining Cadaster portal)	Shilingi elfu moja (1,000)	<p>Kuidhinishwa kwa kukataliwa kwa leseni katika siku tisini</p> <p>Arifa kwa mwombaji kukubali ama kukataa/kughairi</p> <p>Leseni kutolewa kwa muda wa siku ishirini na moja (21) baada ya kuchapishwa</p>

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
8.	Leseni ya mwaka mmoja kwa wafanyabiashara wa madini (muda wa leseni huisha tarehe 31 mwezi wa Disemba)	Tuma maombi kwa kutumia fomu rasmi na kutoa ushahidi wa tajriba, ujuzi na rasilimali	Shilingi elfu ishirini (20,000)	Kuidhinishwa ama kukataliwa kwa muda wa siku mia moja ishirini (120) baada ya barua ya maombi Arifa kabla ya siku thelathini (30) baada ya kutolewa idhini Leseni kutolewa katika siku arobaini na tano (45) baada ya kuchapishwa kwenye gazeti rasmi la serikali na magazeti ya kila siku nchini
9.	Kibali cha kuuza madini nje ya nchi	Tuma ombi kwa kutumia fomu rasmi	Shilingi elfu mbili (2,000)	Siku saba (7)

Nambari	Huduma inayotolewa	Majukumu/Wajibu wa Mteja	Malipo/Ada	Muda wa kutoa Huduma
10.	Upimaji na uchambuzi wa sampuli katika maabara	Wasilisha sampuli kwenye maabara yetu yaliyo katika jumba la madini (Madini House), Nairobi	Shilingi mia tano (500) kwa kila uchunguzi	Kati ya siku tatu (3) na kumi na nne (14) rasmi za kazi
11.	Kibali cha uagizaji/uuzaji wa vilipuzi nje ya nchi	Wasilisha fomu rasmi ya maombi	Hakuna malipo	Siku mbili (2)

Tovuti: www.petroleumandmining.go.ke **Tovuti: www.petrolinamadini.go.ke**

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na : ps@petroleum.go.ke
ps@mining.go.ke